## Maswali

1. Nini ilipatikana kwa mfuko wa Benyamini?
2. Ndoto ya Yusufu ilitimizwa namna gani?
3. Yuda alijitoa kufanya nini?
4. Mbona nduguze Yusufu waliogopa alipowambia yeye ni Yusufu?
5. Mbona Yusufu alisema alikuwa ametumwa Misri?
6. Farao alikaribisha familia ya Yusufu wafanye nini?
7. Mungu aliahidi Yakobo nini?
8. Farao alipea familia ya Yusufu eneo gani ya nchi?
9. Yakobo alipelekwa wapi kuzikwa?
10. Mbona Yakobo alitaka kuzikwa huko?

## Majibu

1. Kikombe cha Yusufu cha fedha kilipatikana kwa mfuko wa Benyamini.
2. Ndoto ya Yusufu ilitimizwa wakati ndugu zake walimwinamia.
3. Yuda alijitoa kubaki gerezani badala ya Benyamini.
4. Nduguze walidhani Yusufu atawaua.
5. Yusufu alisema Mungu alikuwa amemtuma Misri kuokoa watu kutoka kwa njaa.
6. Farao alikaribisha familia ya Yakobo waje waishi Misri.
7. Mungu aliahidi kulinda familia ya Yakobo watakapokuwa Misri. Atamuona Yusufu tena.
8. Farao alipea familia ya Yusufu eneo la Gosheni kuishi.
9. Yakobo alipelekwa kuzikwa Kanaani kwenye Ibrahimu na Isaka walizikwa.
10. Yakobo alitaka azikwe kwa hiyo nchi ili afufuliwe kwa nchi Mungu alimuahidi – wakati Yesu atakaporudi.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1

# 15 Familia ya Yusufu inakuja Misri

**Kwa Biblia** Mwanzo mlango wa 44, 45 na 46:1—7

### Kiini cha somo


Kuonyesha kwamba Mungu anataka tusamehe wenzetu. Kuonyesha upendo wa Mungu na tusaidie watu wake.

### Somo

Simeoni alitolewa kwa gereza. Yusufu na ndugu zake wakala chakula pamoja. Lakini Yusufu hakuwambia kwamba yeye ni Yusufu. Hawakumtambua. Mtumishi aliwajazia chakula kwa mifuko yao ili wapeleke nyumbani. Yusufu alimwambia mtumishi arudishe pesa zao zote kwa mifuko yao. Tena Yusufu akaambia mtumishi aweke kikombe chake cha fedha ndani ya mfuko wa Benyamini.

Ndugu walianza safari ya kwenda nyumbani. Walikuwa na furaha sana. Simeoni alikuwa pamoja nao tena Benyamini alikuwa salama. Lakini kabla waende mbali, mtu aliwafuata mbio.

“Mmeiba kikombe cha mtawala,” aliwapasia sauti. Ndugu walibabaishwa sana. Walijua hawajaiba kikombe. Walijibu, “Hatujaiba kitu chochote. Sisi ni waaminifu. Kuja utupekue.” Waliweka mifuko yao chini na huyu mtu akapekua. Ndugu waliogopa walipoona pesa zao zote ziko kwa mifuko yao. Mtu huyo alipata kikombe ndani ya mfuko wa Benyamini.



Ndugu walirudi kwa nyumba ya mtawala. Walimwinamia Yusufu wote. Walimuogopa. Unakumbuka ndoto za Yusufu kwamba ndugu watamwinamia? Ndugu waliinamia Yusufu huko Misri. Mungu alitimiza hizo ndoto.

Yusufu aliambiwa kwamba kikombe chake kilipatikani ndani ya mfuko wa Benyamini. Yusufu aliamrisha Benyamini awekwe gerezani. Ndugu wengine waende. Yuda alienda chini kwa magoti. Akamsihi Yusufu. Akamwambia kwamba baba yao atakufa kama hawataenda na Benyamini nyumbani. Yuda alisema wamweke yeye gerezani badala ya Benyamini. Hapo Yusufu akakundua kwamba ndugu zake walikuwa wamebadilika. Walikuwa wazuri sasa.


Yusufu aliwambia wajakazi wake wote watoke nje ya chumba. Alianza kulia. Halafu akawazungumuzia nduguze. Akisema, “Mimi ni Yusufu. Baba yangu angali hai?” Ndugu zake wakaogopa Yusufu. Walikumbuka maovu na mabaya yote waliyomfanyia na hata kumuuza kama mtumwa. Walidhani kwamba Yusufu angewaua.

Yusufu aliwambia, “Kuja karibu na mimi. Mimi ni Yusufu mliyemuuza hapa Misri. Msiwe na uchungu. Ni Mungu ndiye alinituma hapa. Mungu alijua kutakuwa na njaa. Mungu alinituma mimi hapa ili niokoe watu kutokana na njaa na kuwa mtawala wa Misri. Yalikuwa mapenzi ya Mungu kwamba mimi nikuje hapa.
Halafu Yusufu akawasamehe nduguze. Aliwabusu kila mmoja na kuwazungumuzia vizuri.

Farao alifurahi aliposikia ndugu wa Yusufu wamekuja Misri. Farao aliwakaribisha wakuje wakae Misri kwa mda wote wa njaa na wakae mahali watataka.

Farao aliwapa magari mengi kwenda kuleta baba yao na familia zao. Aliwapa chakula cha kutumia kwa safari yao ndefu.

Ndugu walirudi nyumbani na habari njema. Yakobo hakuamini kwamba mwanawe mpendwa Yusufu alikuwa angali hai. Lakini alipoona magari na vyakula, aliamini kwamba ni ukweli. Yakobo alipojua kwamba Yusufu ako hai, alifurahi sana. Alikubali waenda wote Misri na waishi wakati wote wa njaa.



Yakobo na familia yake walijipanga kusafiri kuende Misri. Kulikuwa na shuguli na juhudi nyingi. Yakobo alikuwa na uoga kidogo - alikuwa haki kuacha nchi yenye Mungu alimuahidi yeye pamoja na Ibrahimu na Isaka? Mungu akamzungumuzia Yakobo kwa ndoto.

Yakobo alifuhi sana. Mungu atamlinda na amuone Yusufu tena. Yakobo na familia yake walisafiri kwenda Misri. Familia yao yote walikuwa watu 70. Yakobo na Yusufu walifurahi sana kuonana tena.

Huko Misri, Farao alimpa Yakobo na familia yake eneo la Gosheni kuishi. Gosheni ilikuwa na nyasi nzuri kwa mifugo yao. Yakobo na familia yake walikuwa na chakula kingi wakati wa njaa. Waliishi vizuri huko Gosheni. Yakobo alipokufa, alipelekwa kuzikwa kwa nchi ya Kanaani. Alizikwa pamoja na Ibrahimu na Isaka. Yakobo alijua kwamba atafufuka kwa wafu na ataishi kwa nchi waliyoahidiwa na Mungu. Alitaka azikwe kwa hiyo nchi ili ajitayarishie hiyo siku.